# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI

TOLEO MAALUM

ISSN 2507 - 797X Toleo Maalum No 02 2023/2024

# MIAKA 62 YA UHURU NA KINONDONI YA KIJANI



## TUNZA MAZINGIRA KWA MANUFAA YA VIZAZI VIJAVYO







MIAKA 62 YA UHURU TUMEBORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU, AFYA KILA KATA





MIAKA 62 YA UHURU TUMEBORESHA MIUNDOMBINU YA BARABARA

TUMEWASIKIA, TUMEWAFIKIA     MIAKA 62 YA UHURU

MHARIRI MKUU
AQUILINUS SHIDUKI

MHARIRI MSAIDIZI
BEATHA SINGANO

WAPIGA PICHA
KAUNGA MAULID
FILBERT ODILO

MSANIFU JARIDA
JAMILA MDEMU

WAANDISHI
ATHUMAN NTAFUMILA
DIANA MMARY
KAUNGA MAULID

JARIDA HILI LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI
S.L.P, KINONDONI, 31902 DSM
SIMU: +255222170173
BARUA PEPE: md@kinondonimc.go.tz



# TAHARIRI

## MIAKA 62 YA UHURU: KINONDONI YAZIDI KUIMARIKA

LEO, Disemba 9, 2023 Taifa letu linatimiza miaka 62 tangu kuasisiwa kwake. Katika kusherehekea umri huu wa Taifa letu, sisi Manispaa ya Kinondoni kwanza tunatoa salamui za pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuliwezesha Taifa hili kuzidi kushikamana, kuwa Taifa lenye Amani na upendo mingoni mwa wananchi wake na hata majirani zetu. Tunasema asante Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha Amani, Umoja na Mshikamano.

Sisi Manispaa ya Kinondoni, tunaadhimisha kumbukumbu hii huku tukitafakari mambo makubwa ya kimaendeleo yaliyofikiwa katika kipindi hiki hususan ndani ya miaka Mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan. Tumeshuhudia hatua kadhaa za uimarishaji miundombinu ya utoaji wa huduma za Afya, Elimu, Miundombinu pamoja na uwezeshwaji wananchi kiuchumi ukikua kwa kasi kubwa ndani ya Manispaa yetu.

Chini ya Uongozi mahiri wa Mstahiki Meya wa Manispaa, Mheshimiwa Songoro Mnyonge, Baraza la Madiwani, Mkurugenzi wa Manispaa, Bi. Hanifa Suleiman Hamza, Wakuu wa Idara na Vitengo vya Manispaa tumeendelea kuona juhudi na matunda ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha miundombinu hiyo.

Tumeona Awamu ya Sita ikitoa zaidi ya shilingi Bilioni 5.1 katika kuboresha miundombinu ya Elimu na Elimu Sekondari. Juhudi zote hizi ni kuweka mazingira bora ya kujifunza na kufundishia. Kwa sasa Manispaa ya Kinondoni, tunaendelea kujivunia kuwa na shule za Sekondari 34 na tumeanza ujenzi wa Sekondari ya Kata ya Tandale.

Kwa upande wa Afya, hadi sasa Serikali ya Awamu ya Sita imeiwezesha Manispaa hii kuwa na vituo 35 vya kutolea huduma za afya. Vituo hivi ni Zahanati 25, vituo vya Afya Tisa na Hospitali Moja na ununuzi wa magari mawili ya wagonjwa. Aidha, Manispaa ya Kinondoni pia, imewezesha wananchi kiuchumi kupitia vikundi 4,426 vya wajasiriamali kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 17.8.

Mwelekeo wa Manispaa yetu ni kujikita katika Uchumi wa Buluu. Tunapojiandaa kusherehekea miaka 63 ya uhuru, Sisi Manispaa ya Kinondoni tunalenga kuingia katika Uchumi wa Buluu kwa kasi zaidi. Tunatumia fursa hii, kuwaalika wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kuja kuwekeza Kinondoni katika sekta m,balimbali za Uchumi wa Buluu.

Tunazidi kutoa pongezi nyingi kwa Serikali katika miaka hii 62 ya Uhuru na tuna matumaini makubwa ya mafanikio sisi Wana Kinondoni katika uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ya huduma za jamii na kiuchumi kwa kuhakikisha inasukuma mbele ajenda ya kuweka mazingira bora ya upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi zitakazotuwezesha kuendelea kutoa hduma bora kwa wakazi wa Manispaa ya Kinondoni.

#miaka62yauhurukaziiendelee.



# KINONDONI YA KIJANI TUMEJIDHATITI

Na
**ATHUMAN NTAFUMILA**

Manispaa ya Kinondoni kupitia Kitengo Cha Usimamizi wa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira imejidhatiti kwa kutoa elimu juu ya utunzaji na uhifadhi wa maliasili na mazingira kwa kutoa elimu katika Kata zote za Wilaya ya Kinondoni.

Hayo yamebainishwa na Afisa Mazingira wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bw. Awadh Jambo wakati akiongoza zoezi la utoaji elimu ya utunzaji wa mazingira katika kingo za mito ili kuepukana na changamoto za mafuriko zinazoendelea kutokea.

"Katika kipindi chote hiki cha mvua ambazo zinaendelea kunyesha tunatakiwa kuchukua tahadhari madhubuti kwa kupanda miti katika kingo za mito na sehemu zote ambazo zina changamoto kubwa ya kuharibiwa na mvua na tukifanya hivyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza na kumaliza kabisa madhara ya mafuriko," amesema Bw. Awadhi.

Lakini pia Bw. Awadhi amewasa wananchi wote wanaioishi pembezoni mwa mito hasa katika kingo ambazo zimeoneka kuwa athari kubwa kuwa makini zaidi kwa kupanda miti ambayo itawasaidia kuzuia madhara yatokanayo na mvua.



*Afisa Mazingira wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bw. Awadh Jambo, akiongoza zoezi la utoaji elimu ya utunzaji wa mazingira katika kingo za mito ili kuepukana na changamoto za mafuriko zinazoendelea kutokea.*

Aidha Afisa Mazingira huyo amesema kuwa hadi kufikia siku ya maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru Manispaa ya Kinpondoni itakuwa imefanikiwa kupanda miche ya miti zaidi ya 2000 katika kingo na kwenye makazi.

Mbali na hayo pia Bw. Awadhi amesema kuwa kufuatia zoezi hilo la upandaji wa miti wataweka sheria kali dhidi ya waharibifu wa miti hiyo na mifugo hasa mbuzi ambao wameonekana kula miti inayopandwa.

"Tumedhamiria kuiweka Kinondoni ya kijani kwa kuanzisha kampeni ya upandaji wa miti katika maeneo yote ya kingo za mito na kwenye makazi na hii ni kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassani ya utunzaji wa mazingira," amesema Bw, Awadhi.



Nae Gibson Kaiza, kutoka Kitengo Cha Usimamizi wa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira Manispaa ya Kinondoni anasema suala la mifugo kula miti inayopandwa inasababishwa na wananchi wenyewe kutokuwa makini kuilinda na kuwakataza wanaochunga mbuzi katika maeneo ya miti.

Pia Bw. Kaiza amesema kuwa endapo watashirikiana kwa ukaribu zaidi na kuwajibika tatizo la miti kuharibiwa na mifugo halitakuwepo tena kwani hata hivyo sharia ya ufugaji mjini inamtaka mfugaji afugie mifugo ya ndani na sio kuitoa nje.

Aidha, Bw. Kaiza amewasihi Wananchi kuwa walinzi wema wa Mazingira na kingo za mito kwa kupanda miti na kutoa taarifa kwa wale wanaowakwamisha juhudi za upandaji wa miti katika kingo na makazi.

# KINONDONI KUPANDA MITI ZAIDI YA 2000

**Na**
**ATHUMAN NTAFUMILA**




***Afisa Mazingira wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bw. Awadhi Jambo (kulia) akipokea miche ya ya miti iliyopandwa katika maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru***

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kupitia Kitengo Cha Usimamizi wa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira imefanikiwa kupanda miche ya miti zaidi ya 2000.

Akiongea katika zoezi hilo Afisa Mazingira wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bw. Awadhi Jambo amesema Manispaa ya Kinondoni imekuwa na utamaduni wa kuazimisha siku hii ya Uhuru kwa kupanda miti katika maeneo mbalimbali ikiwepo pembezoni mwa barabara na kwenye kingo za mito, ikiwa na lengo la kutunza Mazingira.

Bw, Awadhi amesema kuwa hii ni moja ya njia madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi katika kutunza Mazingira kwa kupanda miti ya kutosha ambayo ni msaada mkubwa katika kupunguza hewa ya ukaa.

Afisa Mazingira huyo amesema kuwa ufugaji wa mifugo mijini usiofuata taratibu imekuna ni kikwazo kikubwa cha ukuaji wa mityi inayopandwa kwenye kingo za mito na pembezoni mwa barabara.

Aidha Bw. Awadhi asilimia kubwa inayopelekea miti mingi inayopandwa kupotea ni Wananchi wanaofuga kiholela pasi na kufuata utaratibu na sheria za ufugaji mijini, kwani kuna miti iliyopandwa kwenye taasisi kama vile Shule na Sehemu za Huduma za Afya kumekuwa na mafanikio makubwa sana kutokana na usimamizi na ufuatiliaji mzuri katika maeneo hayo.

"Wananchi na jamii kwa ujumla watambue kuwa nguvu na gharama kubwa inatumika kuhakikisha mbegu za miche mbalimbali zinaandaliwa mpaka kufikia hatua ya kupandwa katika maeneo husika na vivyo hivyo tumejipanga kutumia nguvu na gharama kuwashughulikia wakwamishaji wa zoezi hili hususani wafugaji wanaoacha mifugo yao izurule hovyo na kutuharibia miti" ameongeza Awadh.

Manispaa ya Kinondoni kupitia Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira imejipanga kuhakikisha inapata mwendelezo mzuri wa upandaji wa miti Ili kufikia malengo bainifu ya kulinda na kutunza Mazingira, Ili kufikia hayo Kuna mipango mikakati itafanyika kwa wale ambao wamekuwa kikwazo kwa kuhakikisha Sheria bainifu za Mazingira zinatekelezwa.

Pamoja na kupata faida ya kupendezesha na kutunza Mazingira kupitia miche mbalimbali ya miti inayopandwa, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imejipanga kuhakikisha miti ya matunda pia inapewa kipaombele Cha kutosha Ili Wananchi na Jamii kwa ujumla wapate matunda kwa wingi na kukamilisha mlo kamili yakiwemo matunda mbalimbali.

Mara kadhaa Wananchi wanaoishi karibu na mito wamekumbana na kadhia za kuingiliwa na maji kwenye makazi yao, suala hilo linaweza kuzuilika baadhi ya sehemu ambazo kuna miti na uoto wa kutosha kwenye kingo za mito husika na hii ni faida mojawapo ambayo Manispaa wameona itakuwa tiba ya kuwalinda Wananchi wake, hivyo nao washiriki kila hatua ikiwemo ulinzi wa miche na miti inayopandwa.

Majanga mbalimbali yanayotokea katika jamii, kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na shughuli za kibandamu, hivyo yanaweza kuzuilika kwa kutoa elimu ikiwemo hii ya umhimu wa Mazingira yetu kulindwa na kutunzwa.

# KINONDONI KUSHIRIKISHA WANANCHI USAFISHAJI KINGO ZA MITO

**Na**
**KAUNGA MAULID**

Kufuatia mfululizo wa mvua zinazoendelea kunyesha zikienda sambamba na uharibifu wa mazingira, miundombinu na makazi ya watu, Wananchi wa Kata ya Wazo wameomba kupewa taarifa na ushirikishwaji juu ya uhifadhi na utunzaji unaotakiwa.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kupitia Kitengo Cha Usimamizi wa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira, imeendelea kufanya jitihada za dhati za kuwapatia elimu Wananchi kuhusiana na utunzaji wa Mazingira Ili kuepukana na athari za mabadiliko ya tabia ya Nchi, ambayo yanapelekea adhaa mbalimbali zinazoathiri Mazingira na maisha ya Wanadamu ikiwemo kuharibika kwa makazi.

Shughuli mbalimbali za Kiuchumi kama vile Usafishaji wa mito kwa kuchimba au kuondoa mchanga zinazofanywa na baadhi ya Wananchi ni moja ya sababu zinazopelekea kuharibika kwa Mazingira na maeneo ya karibu na mito hususani makazi ya watu kwakuwa baadhi ya wahusika hawafuati taratibu mahususi zitakiwazo Ili kulinda Mazingira husika.

Wananchi wa Kata ya Wazo hususani Mtaa wa Wazo na Kilimahewa ni wahanga wakubwa waliopata kadhia ya kubomokewa na makazi yao kutokana na shughuli za uchimbaji wa mchanga katika mto Tegeta ambazo pia hazifuati taratibu zilizowekwa na bonde na hata ushauri unaotolewa na Wataalam kutoka Manispaa ya Kinondoni haufuatwi itakiwavyo.



***Moja ya Vikundi vilivyoweza kupata mkopo wa asilimia 10 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni yaani 4% kwa akina mama, 4%kwa Vijana na 2% kwa watu wenye ulemeavu.***

Cassian Ngamilo, mkazi wa Kilimahewa, amesema kuwa moja ya sababu inayopelekea mto Tegeta kuleta athari kwa wakazi wa maeneo ya mto huo ni kutokana na uchimbaji wa mchanga unaofanywa na vijana wanaojitafutia riziki, kwakuwa wanafanya shughuli hiyo bila kuwa na miongozo thabiti na usimamizi mahususi unaotakiwa Ili kuepuka athari zilitwazo na shughuli hiyo.

"Vijana wanaosafisha mto kwa kuchimba mchanga wanafanya jambo la msingi katika kulinda njia za mto, lakini inageuka kuwa kero kwasababu tu hawana usimamizi na miongozo, hali inayopelekea kuchimba hovyo na kuharibu badala ya kutengeneza", anasema Cassian.

Ili kuondokana na adhaa zinazoletwa kutokana na shughuli hizo Wananchi wanaomba kuwepo na ushirikishwaji madhubuti Ili kuwepo na uwazi wa kuwasimamia vijana wanajipatia ridhiki kupitia malighafi hizo za majini.

Gibson Kaiza, kutoka Kitengo Cha Usimamizi wa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira Manispaa ya Kinondoni anasema suala la kuwashirikisha Wananchi ni jambo jema kwakuwa wao wanaweza kujua na kuwatambua wasiofuata au wanaokiuka taratibu stahiki.

Kadhalika, Bw. Kaiza amewasihi Wananchi kuwa walinzi wema wa Mazingira na kingo za mito kwa kupanda miti na kuwachukulia hatua wale wanaowakwamisha kwakuwa hawatoki mbali Bali ni sehemu ya jamii yao.

"Madhara yanapotokea watu huanza kusema tulipanda miti lakini fulani aliachia mifugo yake ikaharibu, lakini swali la kujiuliza ulikuwa wapi kumwambia asifanye hivyo tangu awali?", anasema Bw Kaiza.

Mazingira yetu ni salama yanapotunzwa na kulindwa katika hali itakiwayo kwa wakati husika na sisi ni sehemu yake, tunaposhindwa kuyatunza maana yake tunayaweka rehani maisha yetu sote, kauli ya kwamba tunza Mazingira yakutunze ipewe uzito madhubuti.

# KIWANDA CHA KUCHAKATA MBOJI KIMEPUNGUZA UCHAFUZI WA MAZINGIRA KINONDONI





**Na**
**JAMILA MDEMU**

Katika kuadhimisha miaka 62 ya Uhuru Manispaa ya Kinondoni inaendelea na mchakato wa kusafisha mazingira ambapo Kila mmoja ana jukumu la kuweka mazingira safi hasa usafishaji wa mitaro na mito ili kuepukana na athari zitokanazo na mvua zinazoendelea kunyesha.

Katika kuiendea kilele cha maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru, Kinondoni imeadhimia kufanya usafi eneo la Coco Beach pamoja na Tanganyika Packers ambapo Kila Mwananchi atahusika na zoezi hilo kwani hilo ni zoezi endelevu katika Manispaa ya Kinondoni.

Kiwanda cha kuchakata mbolea asili (mboji) kilichopo Kata ya Mabwepande Manispaa ya Kinondoni kinasaidia sana kuweka Kinondoni safi ambapo kinajihusisha na ukusanyaji wa taka mali ( taka oza) ambazo ni matunda, mbogamboga, mabaki ya vyakula ambazo hugeuzwa kuwa kuwa mbolea asilia.

Akizungumza Afisa Mazingira Manispaa ya Kinondoni Bw. Shedrack Maxmillan amesema, dhumuni la kuanzisha kiwanda hicho ni pamoja na kupunguza tatizo la hewa chafu katika mazingira sambamba na kusaidia taka kutozagaa katika mazingira yetu.

Amesema "kiwanda kimesaidia kuondoakana na hewa chafu, kimepunguza lookuchafuzi wa mazingira masokoni na katika makazi ya watu, kimetoa fursa ya ajira na kimesaidia taka oza kuwa malighafi ambayo ni mbolea asilia (mboji).

Aidha, Bw. Shedrack amesema, kiwanda kimesaidia jamii kuelewa umuhimu wa kutunza mazingira hasa kuelewa kuwa taka oza zinafaa kwa matumizi mengine. "Mwanzoni jamii haikuwa na uelewa juu ya matumizi ya taka oza baada ya kupata elimu taka hizo zinahifadhiwa kwa ajili ya kutengeneza mbolea ya asili (mboji)", amesema Bw. Shedrack.

Ameongeza kuwa, kutokana na uzalishaji mkubwa wa mbolea asilia na elimu itolewayo kuhusiana na umuhimu wa mbolea hiyo masoko yameongezeka na kupelekea kutanua maeneo ya ukusanyaji wa taka oza ambazo ndio chanzo halisi cha mbolea ya mboji na kusaidia kwa kiasi kikubwa kuondokana na uchafuzi wa mazingira.

Miongoni mwa mambo muhimu yanayotakiwa kufanyika siku ya kilele cha kutimiza miaka 62 ya Uhuru ni kuendelea kuboresha miundombinu na kutoa motisha kwa wananchi ili taka oza zisitupwe ovyo kwani zina faida kubwa katika kuzungusha uchumi sambamba na kuzalisha wadudu maalum ambao wanatumika kama chakula kwa ajili ya baadhi ya wanyama, samaki pamoja na ndege.

# VYOMBO VYA HABARI NA MAENDELEO ENDELEVU YA MANISPAA NDANI YA MIAKA 62 YA UHURU

**Na**
**DIANA MMARY**

Tangu uhuru, tasnia ya habari imekuwa muhimu katika kuchangia maendeleo ya Manispaa ya Kinondoni. Vyombo vya habari vimekuwa vikitoa taarifa za kina kuhusu maendeleo ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa katika eneo hilo. Ripoti za habari zimesaidia kuhamasisha umma kuhusu changamoto na fursa zinazojitokeza, huku pia zikiwezesha wananchi kupata habari sahihi kuhusu sera za serikali na mipango ya maendeleo.

Pia, tasnia ya habari imesaidia kukuza demokrasia na uwajibikaji kwa kuchunguza na kuripoti matukio ya kisiasa na utawala. Wanahabari wamekuwa wakicheza jukumu muhimu katika kuelimisha jamii na kusimamia matumizi ya raslimali za umma.




Vyombo vya habari vinachangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya Manispaa ya Kinondoni. Ripoti za habari zinaweza kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo kama usafi wa mazingira na miradi ya kijamii. Pia, vipindi vya elimu kwenye redio na televisheni vinaweza kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu huduma za manispaa na haki zao. Mifano ni pamoja na matangazo yanayoeleza fursa za ajira au miradi inayotekelezwa na serikali katika eneo hilo.

Hata hivyo, kama sehemu nyingine, tasnia ya habari inakabiliwa na changamoto kama vile upendeleo wa kisiasa na kiuchumi, na pia changamoto za kiteknolojia. Jitihada za kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari na kuendeleza weledi zinahitajika ili kuhakikisha tasnia hii inachangia kikamilifu katika maendeleo endelevu ya Manispaa .



# ZOEZI LA USAJILI WATOTO CHINI YA UMRI WA MIAKA 5 UMEANZA KINONDONI

**Na KMC MEDIA**

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeanza zoezi maalumu la usajili wa watoto wenye umri chini ya Miaka mitano. Zoezi hilo la siku 10 tayari limeshaanza leo Desemba 08 hadi tarehe Desemba 17, 2023 na baadae zoezi hilo litaendelea kwa siku 90.

Ikiwa tayari zoezi la usajili wa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) limeanza linatarajiwa kutolewa katika Kata zote 20 za Manispaa ya Kinondoni ikiwa na lengo la kuwafikia watoto wote ndani ya Wilaya ya Kinondoni.

Zoezi hilo linatolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali, vituo binafsi pamoja na Ofisi za watendaji wa Kata zote ndani ya Manispaa ya Kinonodoni.

Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeendelea kuwaomba na kutoa rai kwa wazazi kwenda katika vituo na ofisi tajwa ili kurahisisha zoezi la usajili wa watoto wao.

Lakini pia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imesema kuwa zoezi hilo ni maalumu kwa watoto hao kwa itarahisisha zaidi upatikanaji wa huduma kwa watoto hasa huduma za kiafya, elimu na nyingine nyingi za msingi kwa wattoto hao.

Mbali na hayo pia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imesema kuwa zoezi hilo ni zoezi endelevu kwani imelenga kufikia vituo na ofisi zote za Kata zilizopo ndani ya Wilaya ya Kinodoni.

Hivyo tuendelee kuwasisitiza wazazi na walezi wote kutembelea vituo vya afya vya serikali na binafsi pamoja na ofisi zote za Kata zilizopo manispaa ya Kinondoni.




*Moja ya vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vinatumika katika zoezi la usajili wa watoto katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.*

# MIAKA 62 YA UHURU NA UBORESHAJI WA BARABARA

**Na KAUNGA MAULID**

Ikiwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa Kilomita 0.85 unaendelea katika Kata ya Kijitonyama Kamati ya siasa Mkoa wa Dar es salaam imeridhishwa na kasi ya ujenzi huo.

Akiongea katika ziara hiyo Mwenyekiti wa Kamati ya siasa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Abbasi Mtemvu amesema hii ni zaidi ya utekelezaji kwani ujenzi umetokana na fedha za mapato ya ndani hivyo kasi ya utekelezaji iendelee hivyo hivyo ili mradi uishe kwa muda uliopangwa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule amesema ujenzi wa mradi huo wa barabara wenye urefu wa Kilomita 0.8 ambapo Kilomita 0.2 ni za barabara ya Jamirex (Msikitini), Kilomita 0.25 ni barabara ya Kimbiji, Kilomita 0.2 ni barabara ya Zahanati na Kilomita 0.2 itakuwa katika barabara ya Nakiete.





# TUENDELEE KUCHUKUA TAHADHARI DHIDI YA MVUA ZINAZOENDELEA KUNYESHA

Na
**ATHUMAN NTAFUMILA**

Kamati elekezi ya usimamizi wa maafa kutoka Wilaya ya Kinondoni Ikiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule wameendelea kutoa tahadhari kwa wananchi juu ya mafuriko ya mvua zinazoendelea kunyesha.

Mhe. Mtambule ametoa tahadhari hiyo wakati alipoenda kutembela ujenzi wa daraja linalounganisha eneo la Mbweni Mpiji na Mtaa wa Kiembeni.

Daraja hilo lenye thamani ya shilingi bilioni 18 litasaidia kwa kiasi kikubwa katika uendeshwaji wa shughuli za kimaendeleo ndani ya ilaya ya Kinondoni.

Aidha mbali na hayo pia katika kujiandaa kukabiliana na mvua za Vuli zinazoweza kusababisha El Nino, Manispaa ya Kinondoni imetakiwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi zote ili kuepukana na maafa.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni,





Mheshimiwa Saad Mtambule, katika kikao cha majadiliano namna ya kukabiliana na changamoto za mvua hizo, alisema "Viongozi na wananchi shirikianeni katika kuboresha miundombinu, na mikakati kuzuia maafa tarajiwa."

Hadi sasa, Mitaa 40 kati ya 106 na Kata 16 kati ya 20 zimebainika kuwa hatarini kupata mafuriko. Kata hizo ni Bunju, Kigogo, Magomeni, Mzimuni, Hananasif, Tandale, Kawe na Kijitonyama. Kata nyingine ni Mbweni, Mbezi Juu, Mwananyamala, Makumbusho, Kunduchi, Kinondoni, Mikocheni na Msasani.

Ikiwa ni maandalizi ya kujiandaa na kukabiliana na El Nino, pamoja na mambo mengine, Manispaa inaendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya El Nino huku ikihamasisha watu wanaoishi maeneo hatarishi kuhama.

Hatua nyingine ni kuendelea




kuimarisha barabara, madaraja na kusafisha mifereji na mito mikubwa na midogo ambapo hadi sasa mto Ng'ombe umesafishwa.

Kwa mujibu wa Mratibu na Msimamizi wa Maafa, Bw. Bakari Mlanzi, "Kinondoni imejipanga ipasavyo kukabiliana na maafa ya mvua za El Nino."

Anaendelea kueleza kuwa, "tunaendelea kuhuisha Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Wilaya; tunandaa Mpango wa Dharura wa Kujiandaa na kukabiliana na madhara ya El Nino, kuainisha raslimali zinazoweza kutumiwa katika kujiandaa na kukabiliana na madhara ya El Nino, ikiwepo kuimarisha uwezo wa kutoa huduma za matibabu kwa waathirika, kutambua wadau wa misaada ya kibinadamu, kutambua wadau wakushiriki katika juhudi zinazoendelea za kujiandaa, kupambana na kurejesha hali."

# MATUKIO KATIKA PICHA








**ZOEZI<br>LA<br>UTOAJI DAWA<br>ZA<br>MATENDE<br>NA<br>MABUSHA<br>LINAENDELEA**





## MICHEZO NA BURUDANI KWA WATUMISHI



*Kikundi cha ngoma cha watumishi kutoka Manispaa ya Kinondoni wakikabidhi kombe kwa Mkurugenzi ma Meya wa Manispaa ya Kinondoni.*

**Na KMC MEDIA**

Mtahiki Meya wa Manispaa ya KinondoniMhe. Songoro Mnyonge akiwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza wamekipongeza kikundi cha ngoma cha watumishi kilichoshiriki mashindano ya SHIMISEMITA 2023 Jijini Dodoma.

Pongezi hizo zimetolewa mapema wiki hii wakati wakikabidhi kombe kwa Mkurugenzi na Meya wa Manispaa.

"Ushindi huu umetuletea sifa kubwa hasa katika sekta ya michezo hivyo muendeleze juhudi hizo za kuitangaza Manispaa yetu,"

# MAANDALIZI YA UZINDUZI WA KITUO KIPYA CHA MABASI MWENGE



# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI










*Jarida la Manispaa ya Kinondoni 2023/2024*
*www.kinondonimc.go.tz*